

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

Barua zote zaidikwe na kutumwa kwa:

Simu: +255 659 566703 (Direct line)

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P. 70, SIKONGE
TABORA

Barua Pepe: ded@sikongedc.go.tz

TAREHE: 15/07/2022

TANGAZO

LA

ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA UKUSANYAJI WA TAKA NGUMU KATIKA SENTA ZA BIASHARA NA MAKAZI KATA ZA SIKONGE NA MISHENI - LGA/121/2022 - 2023/NC/05

MARUDIO - 2

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anakaribisha maombi toka kwa Watu binafsi / Vikundi / Wajasiliamali wenye nia na uwezo wa kutoa huduma ya ukusanyaji wa taka ngumu katika Senta za Biashara na Makazi Kata ya Sikonge na Kata ya Misheni.
2. Kazi hii ni kuanzia tarehe 01 September, 2022 hadi tarehe 30 Juni, 2023.
3. Unakaribishwa kuleta Vidadisi bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoielezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II.
4. Vitabu vya vidadisi bei vinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa bei ya Tsh. 15,000/= ambayo haitarudishwa (non - refundable). Mwombaji atalipia kitabu cha Zabuni baada ya kupewa ' Control number / Account number / BILL toka katika Ofisi ya Mwekahazina au Uhasibu na kulipia

5. Vidadisi bei vyote viwe na nakala **HALISI (ORIGINAL)** na **'COPY' MOJA** zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha zilizowekwa kwenye bahasha na juu yake iandikwe kama ifuatavyo;

**"KIDADISI BEI NA. LGA/121/2022- 2023 /NC/05" KUTOA HUDUMA YA
UKUSANYAJI WA TAKA KATIKA SENTA ZA BIASHARA NA MAKAZI KATA ZA
SIKONGE NA MISHENI - LGA/121/2022/2023/NC/05**

6. Maombi yote yapelekwe (yatumwe) **KWA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI
(W) KITENGO CHA MANUNUZI,
S.L.P 70,
SIKONGE.**
7. Mwombaji atafanya kazi ya kuzoa taka katika sehemu za kukusanyia taka (Vizimba)
8. Mwombaji atafanya kazi ya kusafirisha taka na kuzihifadhi
9. Mwombaji atafanya kazi ya kusafisha Mitaro kandokando ya barabara zote
10. Mwombaji atafanya kazi ya kukusanya tozo na ushuru wa huduma ya kukusanya taka kwa niaba ya Halmashauri kwa kutumia POS
11. Mwombaji atalipa fedha ya dhamana ya mwezi mmoja kabla ya kuanza kazi (Performance bond). Fedha hii ilingane na asilimia (%) atakayokuwa anawasilisha Halmashauri kwa mwezi
12. Mwombaji aambatanishe HATI ya kuandikishwa kwa Kikundi chao
13. Mwombaji atakayepata kazi hii atawasilisha makusanyo yote Halmashauri, na kiasi cha asilimia 10% kitarejeshwa kwake
14. Mwombaji anatakiwa afanye utafiti kwenye maeneo husika kabla ya kuwasilisha maombi ya zabuni anayoomba
15. Maelezo mengine ambayo mwombaji angepaswa kuzingatia yanapatikana katika kabrasha la zabuni
16. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Vidadisi bei ni **siku ya JUMATATU tarehe 01 .08. 2022 saa 5:00 Asubuhi**. Vidadisi bei vitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi mdogo uliopo katika jengo la Idara ya Elimu Sekondari

17. Vidadisi bei vitakavyochelewa, sehemu ya vidadisi bei, vidadisi bei vya kielektroniki, na vidadisi bei visivyofunguliwa katika tukio la ufunguaji, kwa hali yoyote ile vidadisi bei hivyo havitakubaliwa kwa tathmini.

JINSI YA KUFANYA KAZI

- i) Wakala atapewa na Halmashauri mashine ya kukusanyia ushuru (POS) na wakati wote wakala atahakikisha anatumia mashine hiyo
- ii) Wakala atalipwa asilimia ya makusanyo yake baada ya kuwasilisha makusanyo yake yote kwa mwezi
- iii) Gharama ya kulipa wafanyakazi wake ni juu ya Wakala mwenyewe
- iv) Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha kufanyia kazi anayoomba
- v) Gharama ya usafishaji na usafirishaji wa taka ni juu ya Wakala mwenyewe



Hashim M. Kazoka

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SIKONGE**

WAKURUGENZI MTENDAJI

WILAYA - SIKONGE